**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

# YAH: KUONGEZA MUDA WA KUOMBA NA KUPOKEA MAOMBI YA KAZI (AJIRA YA MUDA)

Kupitia Tangazo lililotolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi la nafasi za kazi **124** za fani mbalimbali la tarehe 7 Juni, 2023, watakaofanya kazi katika Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (**Land Tenure Improvement Project**) kwa malipo ya siku katika maeneo ya Chalinze, Kigoma na Dodoma. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi imesogezwa mbele badala ya tarehe 25 Juni, 2023 sasa itakuwa tarehe **1 Julai, 2023**, kwa nafasi zote zifuatazo;

**NAFASI: AFISA MIPANGO MIJI**
IDADI : NAFASI 23
**AINA YA AJIRA:** Mkataba Muda Maalum
**ENEO LA KAZI**: Dodoma Jiji (08), Kigoma Ujiji (08) na Chalinze Mji (07)

A. **Sifa za waombaji:**
1. Awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18
2. Awe tayari kufanya kazi katika Halmashauri husika
3. Awe na elimu/ujuzi wa angalau shahada ya kwanza katika fani ya Mipango Miji na Vijiji kutoka katika Chuo chochote kinachotambulika na Serikali
4. Awe na uwezo wa kutumia Q GIS au Arc GIS katika kuandaa michoro ya mipango Miji
5. Awe na uzoefu usiopungua miaka miwili (2) wa kufanya kazi za urasimishaji

**MAJUKUMU**

1. Kukusanya Taarifa za uwandani
2. Kupanga maeneo ya urasimishaji
3. Kutoa elimu ya masuala ya kupanga makazi holela
4. Kuandaa michoro ya Mipangomiji
5. Kuwasilisha (Public Display) Michoro
6. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na msimamizi wake

**NAFASI: MRASIMU RAMANI (MAPPING OFFICERS)**
IDADI: NAFASI 5
**AINA YA AJIRA:** Mkataba Muda Maalum
**ENEO LA KAZI**: Dodoma Jiji (02), Kigoma Ujiji (01) na Chalinze Mji (02)

**SIFA ZA WAOMBAJI**

1. Awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18
2. Awe tayari kufanya kazi katika Halmashauri husika
3. Awe na elimu/ujuzi wa angalau shahada katika fani zinazoendana na sekta ya ardhi kutoka katika Chuo chochote kinachotambulika na Serikali
4. Awe na uwezo wa kutumia Auto CAD, Q GIS au Arc GIS katika kuandaa michoro ya mipango Miji
5. Awe na uzoefu usio pungua miaka miwili katika kuandaa ramani

**MAJUKUMU**

1. Kukusanya Taarifa za uwandani na kuunganisha maumbo kutoka kwa wapima/wapima wasaidizi
2. Kuandaa ramani za upimaji/mipango miji
3. Kuwasilisha (Public Display) na kufanya marekebisho kwa kuzingatia maelekezo
4. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na msimamizi wake

**NAFASI: MPIMA AU FUNDI SANIFU MPIMA**
IDADI : NAFASI 24
**AINA YA AJIRA:** Mkataba Muda Maalum
**ENEO LA KAZI**: Dodoma Jiji (08), Kigoma Ujiji (08) na Chalinze Mji (08)

**SIFA ZA WAOMBAJI**

1. Awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18
2. Awe tayari kufanya kazi katika Halmashauri husika
3. Awe na elimu/ujuzi wa angalau stashahada katika fani ya Upimaji ardhi kutoka katika Chuo chochote kinachotambulika na Serikali
4. Aweze na uwezo wa kutumia Auto CAD, Q GIS au Arc GIS katika kuandaa michoro ya upimaji
5. Awe na uzoefu usio pungua miaka miwili wa kufanya kazi za Urasimishaji
6. Awe amehusishwa katika kazi ya upimaji ya viwanja visivyopungua mia tano

**MAJUKUMU**

1. Kukusanya Taarifa za uwandani
2. Kupima maeneo ya urasimishaji
3. Kutoa elimu ya masuala ya kupanga makazi holela
4. Kuandaa michoro ya upimaji na kufunga hesabu za upimaji
5. Kuwasilisha (Public Display)
6. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na msimamizi wake

**NAFASI: WAKUSANYA TAARIFA ZA WAMILIKI VIPANDE VYA ARDHI (PARA SURVEYORS)**

IDADI: NAFASI 24

**AINA YA AJIRA:** Mkataba Muda Maalum

**ENEO LA KAZI**: Halmashauri ya Jiji la Dodoma (08), Halmasahuri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji (08) na Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze (08)

**SIFA ZA WAOMBAJI**

1. Awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18
2. Awe tayari kufanya kazi katika Halmashauri husika
3. Awe na elimu/ujuzi wa angalau Stashahada katika fani zinazohusiana na ardhi kutoka katika Chuo chochote kinachotambulika na Serikali
4. Aweze kutumia vifaa vya kisasa (mobile devices) kukusanya taarifa za wamiliki wa Ardhi na kijiografia
5. Uwezo wa kutumia mifumo ya kijiografia (GIS)
6. Mwenye stashahada ya mipangomiji atawepewa kipaumbele

**MAJUKUMU**

1. Kukusanya taarifa za vipande vya ardhi katika maeneo ya urasimishaji.
2. Kuchukua taarifa za matumizi ya ardhi
3. Kuchukua taarifa za umiliki wa vipande vya ardhi.
4. Kuchakata taarifa zilizokusanywa.
5. Kushirikiana na kamati za urasimishaji katiaka kuwafikia wananchi ili kuchukua taarifa za vipande vya ardhi.
6. Kutunza vifaa vya ukusanyaji taarifa.
7. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na msimamizi wake

**NAFASI: MSADIZI WA UPIMAJI (FIELD ASSISTANT)**

IDADI: NAFASI 48

**AINA YA AJIRA:** Mkataba Muda Maalum

**ENEO LA KAZI**: Halmashauri ya Jiji la Dodoma (16), Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji (16) na Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze (16)

**SIFA ZA WAOMBAJI**

- Awe Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea
- Awe anajua kusoma na kuandika
- Mwenye uzoefu wa kusaidia wampima ardhi katika usimikaji wa vigingi
- Aliyefanya kazi ya usaidizi wa wapima ardhi katika Halmashauri husika atapewa kipaumbele

**MAJUKUMU**

1. Kusaidia katika kubeba vifaa vya upimaji katika maeneo ya urasimishaji.
2. Kuwasaidia wapima katika kuweka alama za mipaka ( Becons ).
3. Kupanga beacons katika mpangilio stahiki
4. Kutekeleza majukumu mengine kadri ya maelekezo ya viongozi wa mradi.

**NAMNA YA KUTUMA MAOMBI**

1. Waombaji wa Dodoma wawasilishe maombi yao katika Ofisi za Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi zilizopo katika Jengo la Kambarage – Dodoma (ghorofa ya kwanza mkabala na CRDB Bank)
2. Waombaji wa Chalinze na Kigoma wawasilishe maombi yao katika Ofisi ya Halmashauri husika (Chalinze na Kigoma Ujiji)
3. Pia maombi yanaweza kuwasilishwa kupitia barua pepe **pc.ltip@lands.go.tz**

Maombi yote yaelekezwe kwa anuani ifuatayo;

Katibu Mkuu,
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,
S. L. P 2908,
**40477 DODOMA.**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 01 Julai, 2023 saa 06:30 mchana.**

NB: Waombaji wabainishe maeneo wanayoomba kufanya kazi

**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**26 JUNI, 2023**